**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 2 No. 2 (2024): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v2i2.863
*Majuto ni Mjukuu: Uchunguzi wa Mhusika Ngoma katika Riwaya ya Ua la Faraja*

# *Majuto ni Mjukuu*: Uchunguzi wa Mhusika Ngoma katika Riwaya ya *Ua la Faraja*

**Adria Fuluge**

*Chuo Kikuu Mzumbe, Tanzania*

***Article History***
Received: 22.10.2024
Revised: 11.12.2024
Accepted: 16.12.2024
Published: 22.12.2024

**Keywords**
Majuto
Methali
Mhusika
Mjukuu

***How to cite:***
Fuluge, A. (2024). *Majuto ni Mjukuu*: Uchunguzi wa Mhusika Ngoma katika Riwaya ya *Ua la Faraja*. *Journal of Linguistics, Literary and Communication Studies, 3*(2), 52-60.

Copyright © 2024
CC BY NC SA

**Abstract**
Maisha ya mtu ni hadithi inayopaswa kusimuliwa ili kutoa mafunzo kwa jamii kuhusu mapito ya mhusika. Hii inatokana na ukweli kwamba kila mtu katika jamii ana mambo mazuri na/au mabaya ya kusimulia yanayohusu mapito ya maisha yake. Yapo masimulizi yanayofurahisha kutokana na matendo ya mhusika na mengine husikitisha kiasi cha kumfanya mhusika kuyajutia maisha yake kutokana na kufanya au kutofanya jambo fulani. Kwa msingi huo, makala hii ililenga kuchunguza methali inayosema "majuto ni mjukuu" kwa kuchunguza maisha ya mhusika Ngoma katika riwaya ya *Ua la Faraja* (2004). Mhusika huyu ameteuliwa kama kiwakilishi cha wahusika wengi ambao katika maisha yao, walifanya na/au hawakufanya mambo fulani ambapo kutokana na kufanya na/au kutokufanya kwao, kulisababisha majuto katika maisha yao. Pia, riwaya hii imeteuliwa kama sampuli ya riwaya mbalimbali zenye wahusika wenye sifa kama za mhusika Ngoma. Data zilitokana na uchambuzi wa riwaya ya *Ua la Faraja*. Vilevile, Nadharia ya Uhalisia ilitumika kama mwongozo katika ukusanyaji wa data, uchambuzi na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti wa makala hii. Matokeo yanaonesha kwamba ziko sababu kuu nne zilizosababisha Ngoma ayajutie maisha yake. Sababu hizo ni kukosa uaminifu katika ndoa, kuitelekeza familia yake, kuendekeza anasa, na kutowajali ndugu zake.

## Introduction

Kwa kawaida msanii wa kazi ya fasihi, hutunga kazi yake kisanaa kwa kuzingatia mambo anuwai anayoyaishi, kuyaona, kuyasikia, kuyaonja, kuyanusa au kuyahisi katika maisha yake, na kuyafikisha kwa jamii husika kupitia kwa wahusika. Wamitila (2003) anaeleza kwamba mhusika ni kiumbe anayepatikana katika kazi ya kifasihi na ambaye anafanana na binadamu kwa kiasi fulani. Maelezo haya yana maana kwamba mhusika hubeba sifa fulani kulingana na dhamira anazopangiwa na msanii ili aziwasilishe kwa jamii husika. Mulokozi (2017) anaeleza kuwa, mara nyingi wahusika katika bunilizi za kawaida ni binadamu, lakini viumbe wa aina nyingine au vitu visivyo na uhai, huweza kutumika pia kutegemeana na fani yenyewe na lengo la mwandishi. Hii ina maana kwamba wahusika ni watu au hata viumbe fulani vinavyochorwa na mwandishi kisanii ili kuwakilisha watu anaowafikiria msanii katika kazi yake. Pia, wahusika ndio watendaji wakuu na kiini cha masimulizi; wao, ndio huibua na kutengeneza tofauti za kimawazo au kimaisha zinazojitokeza baina yao. Kimsingi, msanii huweza kumuumba mhusika kwa kumvisha tabia na

matendo mema ili aweze kuigwa na jamii. Vilevile, anaweza kuwa na matendo mabaya yanayomfanya ayajutie maisha yake, huku akiacha funzo fulani kwa jamii.

Kwa mujibu wa BAKITA (2017), majuto ni jina linalotokana na kitenzi 'juta', yaani hali ya kusikitika kutokana na kufanya jambo lisilokubalika au kutokufanya jambo linalokubalika. Katika maisha, ni kawaida kumsikia mtu akitoa kauli kama vile 'ningejua ningefanya jambo fulani' au 'ningejua nisingefanya jambo hilo'. Katika hali ya kawaida, mtu anapotoa kauli ya "ninge…" huonesha hali ya kujuta kutokana na kufanya au kutokufanya jambo. Aidha, katika Kiswahili zipo methali mbalimbali zinazoonesha namna fulani ya majuto anayoyapata mtu kutokana na kufanya au kutokufanya jambo fulani. Mulokozi (2017) anaeleza kuwa methali ni semi fupifupi zinazoeleza kwa muhtasari fikra au mafunzo mazito yanayotokana na uzoefu wa jamii. Kwa kawaida nguvu ya methali hudhihirika kwa kuzingatia utamaduni na uhalisi wa maisha ya watu (Mieder, 2008). Hii ni kwa kuwa methali ni kauli zilizofinyangwa kutokana na tajriba ya watumiaji. Miongoni mwa methali hizo ni ile isemayo; '*Majuto ni Mjukuu'*. Methali hii inaonesha kwamba katika maisha, binadamu anatakiwa kufikiria na kutafakari matokeo ya matendo anayofanya kwani yanaweza kufanywa au kutokufanywa sasa lakini yakawa na majuto makubwa baadaye. Kimsingi, methali hii inapolinganisha majuto na mjukuu inatoa picha kwamba kama vile mjukuu anavyotokana na vizazi vya awali, majuto nayo ni matokeo ya matendo yetu ya awali.

TUKI (2014) inaeleza kuwa mjukuu ni jina linaloonesha uzao wa tatu kutoka wazazi wa kwanza hadi mwana wa mtoto. Katika lugha ya picha, "mjukuu" anawakilisha kitu ambacho hakiwezi kufutika kirahisi, bali huendelea kuishi na kuzalisha athari za kiakili na kihisia kwa vizazi vyote vya maisha. Kwa kifupi, katika methali hii mjukuu si tu mtoto, bali ni ishara ya kitu kinachokuja kwa kuchelewa, kama vile mjukuu ambavyo huja baada ya vizazi vingine viwili. Kwa msingi huo, methali inayosema majuto ni mjukuu inatupa picha ya matokeo yanayochelewa kufika, kama vile hisia za majuto ambazo mara nyingi hujitokeza baada ya tukio au uamuzi fulani kufanyika. Schlee na Sahado (2002) wanaeleza kuwa methali kama hii inatupa picha ya kifalsafa inayoonesha wakati na hatima ya maisha ya mwanadamu. Pia, huonesha taswira ya mapambano ya kifikra na kihisia inayokuja baada ya mhusika kutambua kuwa wakati unapopita hauwezi kurudi nyuma, badala yake kitu pekee kinachobaki ni majuto. Hii ni kwa kuwa majuto katika uhalisia ni aina ya hukumu ya kibinafsi inayoweza kuharibu au kubadilisha maisha ya mtu kuelekea kwenye mustakabali wake. Kauli hii inathibitishwa na mwandishi wa riwaya ya *Ua la Faraja* (2004) kupitia kwa mhusika Ngoma kama ilivyojadiliwa katika makala hii.

**Muhtasari wa Riwaya Teule**

*Ua la Faraja* (2004) ni mojawapo ya riwaya zilizoandikwa na W.E. Mkufya. Kwa jumla, riwaya hii inasawiri maisha halisi ya Waafrika, hususani Waswahili kwa kuzingatia hali, mitazamo na matamanio yao kupitia kwa wahusika wake. Aidha, mwandishi ametumia mandhari, na lugha inayoakisi utamaduni wa jamii za Kitanzania ili kusawiri hali halisi ya maisha ya jamii hiyo. Vilevile, anaonesha taswira ya mtu anayeendekeza anasa mbalimbali katika maisha yake na athari zitokanazo na anasa hizo kwake na kwa jamii yake, likiwamo suala la maambukizi ya UKIMWI. Kwa kuzingatia hilo, mwandishi anaiasa jamii kuwa maisha ya starehe huweza kuwa chanzo cha kuenea kwa magonjwa mbalimbali. Pia, anabainisha tahadhari zinazopaswa kuzingatiwa wakati wa kufanya tendo la ngono na namna ya kumhudumia mtu mwenye maradhi yanayosababishwa na ngono, hususani UKIMWI. Hii ni kwa sababu ugonjwa huu unawaathiri watu wa rika na makundi yote, bila kujali waliosoma na wasiosoma. Kutokana na hilo, anaitaka jamii ielimishwe kuhusu athari zitokanano na ugonjwa huo ambazo ni pamoja na kurudisha nyuma maendeleo ya familia na jamii, kusababisha msongo wa mawazo, majuto, na vifo. Kwa jumla, kupitia riwaya hii mwaandishi ameweza kuonesha namna mwanadamu anavyoyajutia maisha yake kutokana na matendo yake.

**Nadharia Iliyotumika**

Uandishi na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti wa makala hii uliongozwa na Nadharia ya Uhalisia. Wamitila (2003) anaeleza kuwa uhalisia ni mkondo unaosisitiza usawiri wa matukio au maisha katika fasihi kama yalivyo katika maisha ya kila siku. Hii ina maana kwamba usanii wa matukio katika fasihi unatakiwa kuyafanya matukio hayo yajitokeze kama yalivyo katika jamii kwa kuepuka masuala ya kinjozi, bali kuyaelezea maisha kwa uyakinifu kama yalivyo katika jamii. Kwa mujibu wa Wamitila (2002), Wafula na Njogu (2007), na Mulokozi (2017), nadharia hii iliwekewa misingi na mwanafalsafa George Wilhelm Hegel (1770 – 1831). Baadaye, ilipata nguvu zaidi karne ya ishirini, baada ya wataalamu wengi kuanza kuitumia katika kuhakiki masuala mbalimbali katika jamii zao. Miongoni mwa wataalamu hao ni Karl Marx (1818 – 1883), Maxim Gorky (1868 – 1936), na Georg Lukacs (1885 – 1971). Kwa jumla, Wanauhalisia huamini kuwa kazi ya fasihi inapaswa kusawiri uhalisi katika ukamilifu wake kwa kuchunguza undani wa picha inayoonekana (Wamitila, 2003). Wafula na Njogu (2007) wanafafanua baadhi ya mihimili ya Nadharia ya Uhalisia kama ifuatavyo: Mosi, msanii kuyachora maisha jinsi yalivyo kwa kuhusisha vipengele muhimu vya maisha. Pili, kuwasilisha maudhui ya kazi ya fasihi kwa kuzingatia hali halisi ya jamii. Tatu, wahusika kusawiriwa kiyakinifu ili kuakisi maisha ya kila siku. Hivyo, mihimili hii ilimwongoza mwandishi katika kuchunguza data, kuchambua, na kuwasilisha matokeo ya utafiti wa makala hii.

**Methodolojia**

Makala hii imetumia vipengele mbalimbali vya kimethodolojia ili kufikia malengo yake. Data zilikusanywa maktabani kwa njia ya usomaji wa riwaya ya *Ua la Faraja* (2004). Riwaya hii iliteuliwa kutokana na usomaji wetu wa awali kubaini kwamba ina wahusika wanaoyajutia maisha kutokana na matendo waliyofanya katika maisha yao. Uchanganuzi wa data za msingi ulitumia mkabala wa kitaamuli, ambao huhusisha uchambuzi wa data kwa kutumia maelezo kwa lengo la kufikia matokeo ya utafiti husika (Ponera, 2016). Pia, matokeo ya utafiti huu yalihusisha tafakuri binafsi, data za maktabani, na taarifa mbalimbali za kitafiti. Kwa jumla, Nadharia ya Uhalisia ilituongoza katika kuchunguza na kuchambua data katika riwaya teule kwa kujikita katika mada inayosema 'Majuto ni Mjukuu' huku tukimakinikia mhusika mkuu, Ngoma.

**Matokeo ya Utafiti**

Makala hii imebaini na kujadili sababu kuu nne zilizomfanya Ngoma ayajutie maisha yake kama zinavyojitokeza katika riwaya teule. Sababu hizo ni: kukosa uaminifu katika ndoa, kuitelekeza familia yake, kuendekeza anasa, na kutowajali ndugu zake.

**Kukosa Uaminifu katika Ndoa**

Mlacha (1996) anaeleza kuwa ndoa ni makubaliano rasmi baina ya mwanamke na mwanamume, kwamba wapo tayari kuishi pamoja na kuanzisha familia, ambapo mmoja atakuwa mama na mwingine atakuwa baba katika familia hiyo iliyoanzishwa. Katika makubaliano hayo, mume na mke huwekeana ahadi mbele ya viongozi wa dini, serikali, au viongozi wa ukoo ama wa kimila kwamba wataishi kwa kuheshimiana na kuaminiana ili kujenga familia yenye maadili mema. Hata hivyo, suala la kuishi kwa mujibu wa makubaliano hayo, mara nyingi huwa mwiba, hususani kwa wanaume. Hii inatokana na ukweli kwamba wanaume wengi hukosa uaminifu katika ndoa zao na huanzisha uhusiano wa kimapenzi na wanawake wengine. Mwandishi anathibitisha suala hili kupitia kwa mhusika, Ngoma, anaposema:

> Kutoka siku ile mashaka ya Tabu kuhusu mienendo ya mume wake yaliongezeka mara dufu. Huko nyuma alikwishajua kwamba Ngoma alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Queen. Alikwishawafumania *Kanga Moja Club*. Wakagombana na Queen. Tabu akasusiana na mume wake kwa muda wa karibu juma zima. Wakawa hawaongei wala kusalimiana. Ngoma akamwomba mke wake msamaha,

> akasamehewa. Akaapa kwamba hatarudia tena uhusiano na mwanamke huyo. Kwa shingo upande, Tabu akamwamini… Ndipo katika udadisi huu, akagundua kwamba Queen aliugua Mkanda wa Jeshi, ugonjwa ambao mara nyingi ulisemekana kuwa ni mojawapo ya dalili za UKIMWI (Mkufya, 2004: 39).

Katika dondoo hili, mwandishi anasawiri picha ya matendo ya Ngoma kuhusu uhusiano wake wa kimapenzi na Queen. Siri hiyo inagunduliwa na mkewe na kusababisha mafarakano baina yao. Utafiti wa makala hii umebaini kwamba kitendo cha Tabu kususiana na mume wake na kushindwa kuongea kwa takribani juma moja, kinadhihirisha kwamba kukosa uaminifu katika ndoa ni chanzo kimojawapo cha migongano katika jamii. Kutokana na hilo, Ngoma anatambua kosa lake na kulijutia kwa kumwomba mke wake msamaha huku akiweka ahadi ya kutorudia tena. Hata hivyo, inabainika kwamba Ngoma ameambukizwa UKIMWI ambao ni matokeo ya kukosa uaminifu katika ndoa yake, kwani 'mshahara wa dhambi ni mauti.' Hatimaye, anazidiwa na maradhi hayo kiasi cha kupata shida na kutoa sauti kwa taabu kumwomba tena msamaha mke wake, huku akilia na kuyajutia matendo aliyofanya. Mwandishi anasema:

> Ngoma hakumjibu, sauti ilimkwama. Alikuwa na mengi ya kumjibu mke wake, lakini alikuwa kama amekabwa koo. Sasa hakujali maradhi yake tena. Kilichomuuma ni kule kumwona mke wake na kutokuwa na uwezo wa kujadiliana naye juu ya mifarakano yao. Yeye ndiye aliyekuwa na wajibu wa kumwomba msamaha mkewe. Lakini sasa pumzi ilizuiwa na kichomi alichokuwa nacho. Akabaki akimkodolea macho kama bubu. Machozi yakamtiririka usoni. Hakuweza kujizuia. Alimpenda mke wake, alitamani kumwomba radhi kwa yote aliyomtendea, hasa kule kumsababishia maradhi yatakayosababisha mauti yake. "…Nisamehe mke wangu," alijikusuru kusema na machozi yakatoka tena. Mke wake akayafuta. Ngoma akaendelea, "Nisamehe kwa yote niliyotenda" (Mkufya, 2004: 322 – 323).

Kinachobainika katika dondoo hilo ni kwamba Ngoma yuko katika maumivu makali yaliyosababishwa na matendo yake. Anashindwa kujadiliana na mkewe kuhusu mafarakano yao kutokana na udhaifu wa mwili wake. Kitendo cha baba mzima kulia pasipokutoa sauti kinaonesha namna anavyoyajutia matokeo ya matendo aliyofanya. Kwake, methali inayosema 'Majuto ni Mjukuu' haiashirii tu dhana ya matokeo, bali pia mchakato wa kujifunza kutokana na makosa na umuhimu wa busara na utulivu katika kufanya maamuzi. Wanjohi (2008) na Madumulla (1995) wanaeleza kuwa, kwa makusudi, watu hutumia methali kuwasilisha fikra, imani, na mielekeo yao inayoakisi utamaduni wao. Kwa maana hiyo, methali inayosema 'Majuto ni Mjukuu' inajenga fikra na kumbukumbu ya kudumu kwamba kila tendo lina athari zake. Aghalabu, athari hizo ni za kudumu na zisizorekebishwa. Ithibati ya maelezo hayo inajitokeza kwa Ngoma, kwani haoni tena thamani ya wanawake aliokuwa nao. Badala yake, anarudisha mapenzi yake kwa mkewe huku akieleza kwamba anastahili kumwomba msamaha kutokana na makosa aliyomfanyia, likiwamo la kumwambukiza UKIMWI. Hii ni kwa kuwa, Ngoma hakutaka kuzingatia ushauri aliopewa na mkewe. Akakataa pema pabaya pakamwita. Inaelezwa kwamba:

> Sauti ya Tabu ilianza kukoroma kwa uchungu. Akaendelea kusema huku akilia, "Ngoma! Ngoma! Kwa nini umenihukumu kifo? Nimekukosea nini? Sikukuzalia watoto? Sikuwatunza wanao? Sikukufulia marundo ya nguo? Sikukupokea kitandani hata ukiwa unanuka harufu mbaya za pombe, sigara na majasho ya kilevi? Niambie! Niambie hata siku moja ambayo nilikukosea mpaka sasa nikastahili hukumu hii ya kifo?" (Mkufya, 2004: 35).

Katika nukuu hii, mwandishi anaonesha namna Tabu alivyoumizwa na Ngoma kwa kukosa uaminifu katika ndoa na kumwambukiza UKIMWI. Maumivu yake yanatokana na ukweli kwamba, licha ya mwanamke huyu kumtimimizia mumewe mambo yote yakiwamo ya kumzalia watoto, kumfulia nguo, kutimiza jukumu la ndoa, na kumvumilia aliporudi akiwa amelewa, bado hakuona thamani ya mkewe. Matokeo ya kukosa uaminifu huo ni kuambukizwa UKIMWI, ambapo naye anamwambukiza mkewe. Kimsingi, Tabu analia kwa sababu anabebeshwa adhabu ya kifo asiyostahili. Kwa jumla, Ngoma na Tabu wanasawiri hali halisi ya maisha ya kila siku ya jamii zetu kama inavyoelezwa katika Nadharia ya Uhalisia, kwani ni dhahiri kwamba wanandoa wengi, hususani wanaume wamekosa uaminifu katika ndoa zao. Aghalabu, wamekuwa wakianzisha uhusiano na wanawake wengine na kuwa chanzo cha migogoro katika familia na jamii kwa jumla. Matokeo ya uhusiano huo mara nyingi yamegeuka kuwa shubiri kwao sawa na methali inayosema ‘Majuto ni Mjukuu’.

**Kuitelekeza Familia Yake**

Kwa mujibu wa BAKITA (2017) kutelekeza ni neno linalotokana na kitenzi ‘telekeza’ likiwa na maana ya kutoendelea kutunza vitu, watoto na au watu wanaokutegemea. Kwa maana nyingine, kutelekeza ni kumwacha mtu au kitu bila msaada au uangalizi unaohitajika. Katika riwaya ya *Ua la Faraja*, imebainika kwamba Ngoma aliitelekeza familia yake kwa kuacha kutimiza majukumu ya kuilea. Mwandishi anasema:

> Mwisho wa maelezo hayo, Ngoma aliandika, “Sikutekeleza wajibu alionipa Mungu kuwalea wanangu katika maadili ya dini na kumnyenyekea Mungu. Najitolea mchango huu ili watoto wengine wanaokua walelewe hivyo, wakiwemo wa kwangu wawili: Nuru na Rahma (uk. 321).

Kinachobainika katika dondoo hili ni kwamba, Ngoma anajuta kwa sababu ameshindwa kutekeleza wajibu aliopewa na Mungu wa kulea watoto wake na kuwajengea misingi imara ya dini. Kutokana na hilo, anaiasa jamii isitelekeze familia kama alivyofanya yeye, bali itimize majukumu yake ya kuzitunza kwa kuzingatia maadili na utamaduni husika. Pia, anaonesha mfano kwa kutoa mchango wake kwa ajili ya kuwahudumia watoto mbalimbali wakiwamo wa kwake. Kwa mujibu wa makala hii, Ngoma anafanya hivyo kama sehemu ya majuto kwa jamii yake baada ya kuitelekeza familia yake. Mtoto wake, Juma anachukizwa na kitendo hicho na kukataa kumhudumia katika maumivu yake. Mwandishi anathibitisha:

> Katika siku zake za mwisho, Ngoma alimhitaji sana Juma kwenda kumuuguza. Alikwisha kumtumia watu kwenda kumsihi aje, Omolo akiwa mmoja wao. Pia, aliwatuma wajomba zake Juma: Daudi na Hiza. Lakini Juma alikataa katakata (Mkufya, 2004: 239 – 240).

Dondoo hili linaonesha namna Ngoma anavyopitia wakati mgumu kutokana na kukosa mtu wa kumhudumia katika maumivu yake. Mateso anayoyapata ni matokeo ya kuitelekeza familia yake ambapo hata mtoto wake, Juma, licha ya kutumiwa taarifa kwamba baba yake anaumwa, haoni sababu ya kwenda kumuuguza. Bila shaka, Ngoma anayajutia matendo aliyofanya, yaliyosababisha aitelekeze familia yake, ambayo kwa wakati huo anaihitaji lakini yenyewe haimhitaji. Matokeo yanaonesha kwamba Ngoma alijitahidi kurudisha mapenzi kwa familia yake baada ya kugundua kwamba ameambukizwa UKIMWI, lakini mke na watoto wake hawakuwa tayari kuyapokea mabadiliko hayo. Mwandishi anasema:

> Kila aliporudi toka mjini, Ngoma alijitahidi kuja na kanga, kitenge na nguo mpya kwa ajili ya watoto. Lakini ilimkera kwamba nguo zenyewe hazikuvaliwa. Mke alimshangaa na kusema, “We’ Baba Juma, nguo zote hizi za nini? Mbona hata zile za

> juzi hatujazivaa? Sisi tumezoea: nguo mpya ni wakati wa sikukuu ya Idd. Sasa mtu eti kila leo utoke na nguo mpya, si watu watatushangaa!" (Mkufya, 2004: 151).

Katika maelezo haya mwandishi anaonesha namna Ngoma anavyoyajutia maisha kwa kitendo cha kuitelekeza familia yake. Matokeo yanaonesha kwamba mke na watoto wake walihangaika na kuishi maisha duni kwa muda mrefu, licha ya utajiri aliokuwa nao Ngoma. Ndiyo maana baada ya kubainika kwamba ameambukizwa UKIMWI, anajaribu kubadilika kitabia huku akiiletea familia yake zawadi mbalimbali, zikiwamo nguo. Ama kweli sikio la kufa halisikii dawa, kwani familia hiyo haiko tayari kuvaa nguo zinazoletwa kila leo ilhali yenyewe imezoea kuvaa nguo mpya wakati wa sikukuu ya Idd. Kinachojidhihirisha katika riwaya hii ni kwamba familia ya Ngoma inasawiri maisha halisi ya Kitanzania kama inavyoelezwa katika Nadharia ya Uhalisia kwamba wahusika wasawiriwe kiyakinifu ili kuakisi maisha ya kila siku. Kwa jumla, utafiti wa makala hii umebaini kwamba mwandishi amemtumia Ngoma kama kiwakilishi cha wazazi au walezi wanaoshindwa kutimiza majukumu yao ya kimalezi, hususani akina baba, ambao aghalabu huzitelekeza familia zao kwa kuwaachia majukumu hayo wake zao. Hatimaye, huyajutia matokeo ya matendo yao wanapokumbwa na matatizo, kwa sababu hakuna marefu yasikuwa na ncha, na majuto ni mjukuu.

**Kuendekeza Anasa**

BAKITA (2017) linaeleza kwamba anasa ni mambo au hali ya starehe na raha nyingi. Kwa kawaida, anasa huambatana na mhusika kumiliki mali nyingi kama nyumba kubwa, magari ya kifahari, mavazi ya gharama, na vitu vya kifahari. Mambo mengine ni kula vyakula na vinywaji vya gharama kubwa, na kusafiri katika sehemu za kifahari katika hoteli kubwa na maeneo ya kitalii. Kwa jumla, anasa ni hali ya kuishi maisha ya raha, furaha, na starehe zinazozidi mahitaji ya msingi, ambapo aghalabu, huhusisha matumizi makubwa ya rasilimali. Katika riwaya ya *Ua la Faraja*, Ngoma anasawiriwa kama mhusika anayependa maisha ya anasa huku akikaidi ushauri wa mkewe kuhusu tabia hiyo. Kinywa cha Tabu kinanena:

> "Kila siku nimekuonya: Acha! Acha! Hukunisikia, ulijiona rijali sana kuvamia kila mzoga wa kike ulioukuta. Sasa umeniletea gonjwa. Eti tujadiliane! Nijadiliane na mtu mbaya hata sasa ananuka harufu za uasherati…!" (uk. 34 – 35).

Katika dondoo hili, mwandishi anaonesha namna Ngoma anavyopenda kufanya anasa kwa kutembea na wanawake wengi. Matokeo yake ni kuwa anayajutia matendo hayo anapobaini kwamba ameambukizwa UKIMWI, naye anamwambukiza mke wake asiyekuwa na hatia. Hii ni kutokana na ukaidi wake wa kutosikiliza ushauri aliopewa kuhusu kuacha tabia ya kuendekeza anasa. Ni dhahiri kwamba Ngomba anaposema: "Kwa nini nilifanya uzinzi? Hivi kweli huu ndio mwanzo wangu wa kuelekea kaburini? (uk. 38), anadhihirisha namna anavyoyajutia matendo yake. Kwa wakati huo haoni tena faida yake. Badala yake, anakilaumu kiungo chake cha mwili kilichosababisha apate ugonjwa huo, ambacho hakina nguvu tena, bali kinampa taabu hata wakati wa kujisaidia haja ndogo. Mwandishi anasema:

> "Akafanikiwa kuupata (uume), ndipo akafanikiwa kujisaidia. Alikuwa anawaza na kujuta. Haja iliyotokana na kiungo kile cha mwili ndiyo iliyomsababishia majuto makuu. Alitamani kisingekuweko. Alikichukia, alikichukia. Sasa kiungo kile hakikuwa na umuhimu wowote. Umuhimu ulikuwa kuzaa na kimeutimiza. Amejipatia watoto watano, wametosha. Sasa ni nani aliyeendeleza matumizi ya ziada ya kiungo kile? Ni yeye mwenyewe. Alijilaumu" (Mkufya, 2004: 241).

Dondoo hili linathibitisha kwamba Ngoma yuko katika maumivu makali yanayotokana na kiungo kidogo cha mwili wake, ambacho kwa wakati huo hakina thamani tena kwake. Ithibati ya maelezo hayo inatokana na kauli yake kwamba alitamani kiungo hicho kisingekuweko. Kwa mujibu wa

utafiti huu, maumivu anayopitia yanatokana na tabia yake ya kuendekeza anasa, mchakato wa kufanya anasa, na matokeo ya anasa hizo. Hii ina maana kwamba, majuto yanatokana na mtu kufanya kosa, mchakato wa kufanya kosa, na matokeo yake ambayo ndiyo majuto yenyewe. Hivyo, katika makala hii tunaposema kuwa 'majuto ni mjukuu' tunalinganisha vizazi vinavyotokana na babu, baba, na mtoto, ambapo; Babu anatazamwa kama mkosea, baba ni mchakato wa kukosea, na mjukuu ni matokeo ya kukosea huko. Ufafanuzi huo unalandana na mada ya makala yetu inayosema, 'Majuto ni Mjukuu', ikiwa na maana kwamba anasa alizofanya Ngoma zinalinganishwa na babu, maambukizi ya UKIMWI yanalinganishwa na baba, na matokeo ya maambukizi hayo ni sawa na mtoto. Imebainika kwamba kabla ya kifo chake, Ngoma alifanikiwa kuwaomba msamaha mke na watoto wake huku akiwa katika mateso na maumivu makali. Anasema:

> "Nisamehe mke wangu," alijikusuru kusema na machozi yakatoka tena. Mke wake akayafuta. Na Tabu machozi yakaanza kutoka, lakini hakujali kuyafuta. Ngoma akaendelea, "Nisamehe kwa yote niliyotenda. Waambie watoto wanisamehe." Akaanza kukohoa tena (uk. 322 – 323).

Katika nukuu hiyo, mwandishi anaonesha namna Ngoma anavyoyajutia maisha ya anasa aliyofanya na kusababisha afya yake kuzorota. Anaishia kuomba msamaha kwa mke na watoto wake kwa kitendo cha kuendekeza maisha ya anasa. Kimsingi, kupitia riwaya hii mwandishi anayachora maisha ya Ngoma kwa kusawiri jamii halisi ya mwandishi wa riwaya hiyo kama inavyoelezwa katika Nadharia ya Uhalisia kwamba msanii huwasilisha maudhui ya kazi ya fasihi kwa kuzingatia hali halisi ya jamii husika.

**Kutowajali Ndugu Zake**

Kwa mujibu wa TUKI (2014) 'ndugu' ni jina linalomaanisha mtu aliyezaliwa nawe kwa baba, kwa mama au kwa wazazi wote wawili; ndugu wa damu. Pia, jina hili humaanisha mtu uliyezaliwa naye ndani ya ukoo wako, yaani jamaa wa ukoo mmoja na wewe. Kwa maana ya jumla, ndugu ni mtu aliye na uhusiano wa karibu na mwingine kinasaba, kijamii, au kiimani. Katika riwaya ya *Ua la Faraja*, mwandishi anaonesha kwamba Ngoma hakuwajali wala kuwasaidia ndugu zake walipomwomba msaada wake licha ya kuwa na uwezo wa kufanya hivyo. Kutokana na hilo, nao hawakuwa tayari kumsaidia alipokuwa anaumwa. Mwandishi anaeleza kwamba:

> Ndugu zake Ngoma hawakudiriki hata kuja kumjulia hali. Walidai kwamba huko nyuma Ngoma alikuwa hawajali nduguze. Walimtambua kuwa mtu mwenye pesa nyingi, lakini walipompelekea shida zao hakuwatimizia zote. Wakadhani anawakatili makusudi. Waliposikia habari za ugonjwa wake walisherehekea. "Atakula jeuri yake!" Walisema. "Pesa zake zitamuuguza." (uk. 240).

Katika nukuu hii, mwandishi anaonesha namna kiburi cha mali na uzima kinavyompa jeuri Ngoma. Haoni thamani ya ndugu zake wanapomwomba msaada licha ya kuwa na uwezo wa kuwasaidia. Kwake, thamani yao inaonekana baada ya kuugua na kukimbiwa na marafiki aliostarehe nao. Anawahitaji ndugu zake ilhali wao hawamhitaji wakiamini kwamba 'mchuma janga hula na wa kwao.' Wanadai kwamba "Atakula jeuri yake!" Wanaongeza kwamba "Pesa zake zitamuuguza." Kwa Ngoma, matendo yake yanakuwa ni sawa na majuto ni mjukuu, kwani kitendo cha ndugu zake kukataa kumsaidia akiwa katika maumivu hayo, kinaonesha matokeo ya ubaya aliowafanyia kwa kuringia mali zake. Jambo la kushangaza ni kwamba, hata watoto wake wanafikia hatua ya kumtenga kutokana tabia na matendo yake. Kitendo hicho kinamuumiza zaidi Ngoma na kumfanya ayajutie mambo aliyofanya kabla ya kuambukizwa UKIMWI. Mwandishi anasema:

> Sasa alikuwa kitandani anakohoa na kujutia uhai wake. "Katika watoto wote, Juma nitamlaani mpaka kufa!" Ngoma alijisemea akiwa hapo kitandani amelala. Kilikuwa

> kitanda walichozoea kulala yeye na mke wake. Ngoma alimlaumu mwanawe, Juma, kwa kutokuwepo. Baada ya kuondoka nyumbani miaka minne iliyopita, Juma alikwenda kuishi Buguruni Malapa, kwa babu yake, kwa muda wa mwaka mmoja (Mkufya, 2004: 238 – 239).

Katika dondoo hili, mwandishi anaonesha kwamba Ngoma yuko katika upweke na hakuna mtu anayemjali. Anakohoa na kuteseka akiwa kitandani huku akiyajutia maisha aliyoyapitia. Anaelekeza lawama kwa mtoto wake, ambaye, naye kwa wakati huo haoni sababu ya kuwa karibu na baba yake kutokana na maumivu aliyoisababishia familia yake. Isitoshe, hata mke wake hayupo pamoja naye kwani alishapewa talaka kutokana na kukarahishwa na matendo ya mumewe. Ni dhahiri kwamba Ngoma sasa yuko katika majuto baada ya kufanya kisa kilichogeuka kuwa mkasa kwake. Anawahitaji watu alioona hawana umuhimu kwake. Mwandishi anathibitisha:

> Katika siku zake za mwisho, Ngoma alimhitaji sana Juma kwenda kumuuguza. Alikwisha kumtumia watu kwenda kumsihi aje, Omolo akiwa mmoja wao. Pia, aliwatuma wajomba zake Juma: Daudi na Hiza. Lakini Juma alikataa katakata. (Mkufya, 2004: 239 – 240).

Nukuu hii inaonesha namna Ngoma anavyopitia wakati mgumu kutokana na ugonjwa unaomkabili. Kimsingi, huu ni wakati ambao anahitaji msaada kutoka kwa watu wake wa karibu lakini anaukosa. Aliostarehe nao katika maisha yake hawapo tena upande wake, ndiyo maana anawageukia na kuwaomba msaada watu aliowadharau kwa kuona kwamba hawana thamani kwake. Anauhitaji msaada kutoka kwa mtoto wake, Juma, lakini licha ya kutumiwa taarifa za kuhitajika kwake, anakataa. Kwa wakati huu, Ngoma anajutia laana alizompa mtoto wake. Hili linathibitishwa na mwandishi anaposema: "Ngoma akakaa kimya akikumbuka msururu wa laana zote alizokuwa akimlaani Juma toka siku ile alipokimbilia kwa babu yake" (Mkufya, 2004: 269). Nukuu hii inaonesha kuwa Ngoma anayajutia matendo aliyomfanyia Juma, kwani hakutakiwa kumpa laana. Kwa jumla, mambo aliyoyatenda akiwa na afya njema yanabaki kuwa majuto kwake anapopitia mateso ya kuumwa na kukosa mtu wa kumsaidia. Mwandishi anabainisha hili anaposema:

> Ngoma hakujibu, sauti ilimkwama. Alikuwa na mengi ya kumjibu mke wake, lakini alikuwa kama amekabwa kooni. Sasa hakujali maradhi yake tena. Kilichomuuma ni kule kumwona mke wake na kutokuwa na uwezo wa kujadiliana naye mifarakano yao. Yeye ndiye aliyekuwa na wajibu wa kumwomba msamaha mkewe. Lakini pumzi ilizuiwa na kichomi alichokuwa nacho. Akabaki akimkodolea macho kama bubu. Machozi yakamtiririka usoni (Mkufya, 2004: 322).

Dondoo hili linadokeza namna Ngoma anavyojutia matendo aliyofanya yaliyosababisha aambukizwe UKIMWI. Anakosa nguvu ya kutoa sauti ya kumwomba msamaha mke wake kwa kumwambukiza UKIMWI. Anajuta kwa kuwa hana uwezo wa kujadiliana naye kuhusu matatizo yanayoikumba familia yake. Ni kweli kwamba Ngoma yu dhaifu kiasi cha kushindwa hata kutamka maneno ya kumwomba msamaha mkewe. Kutitirika kwa machozi yake ni kiashiria cha kuyajutia matendo aliyofanya yanayompeleka kwenye kifo. Anajuta kwamba anakikaribia kifo huku akimpenda mke wake ambaye hakumjali alipokuwa na afya njema. Mwandishi anathibitisha kwamba:

> Alimpenda mke wake, alitamani kumwomba radhi kwa yote aliyomtendea, hasa kule kumsababishia maradhi yatakayosababisha mauti yake. Lakini alishindwa kueleza. Tabu akamwendea, akafungua kanga yake na kumfuta machozi. Hakuelewa kwa nini mume wake analia, lakini na yeye huzuni ikamjaa moyoni.

> Kumbukumbu za zamani walipoanza zikajirudia. Akapepesa macho kujizuia na yeye machozi yasije yakamtoka. Sasa kifo kimewakaribia wote na hakuna jinsi yoyote kuweza kuirudisha furaha ile waliyoifaidi ujanani (Mkufya, 2004: 322).

Kinachodhihirika katika nukuu hii ni kwamba, Ngoma yuko katika majuto, kwani anatamani kutua mzigo wa maumivu yake ili amwombe radhi mkewe, lakini inashindikana. Anatambua kwamba mke wake hakufanya makosa yanayostahili adhabu ya kifo. Kitendo cha Tabu kumfuta machozi kwa kanga aliyojifunga, kinaonesha hali ya kukubali kubeba mzigo wa maumivu pamoja na mumewe. Ni ishara ya kumsamehe mume wake kutokana na matendo aliyofanya ambayo matokeo yake ni kifo cha wote wawili. Hata hivyo, mumewe anabaki akijutia namna alivyomtenga na kumwacha akihangaika kulea watoto, huku yeye akifanya starehe na umalaya. Kwa jumla, utafiti huu umebaini kwamba Ngoma ametumiwa na mwandishi kusawiri maisha halisi ya jamii kama isemavyo Nadharia ya Uhalisia kwamba msanii huyachora maisha jinsi yalivyo kwa kuhusisha vipengele mbalimbali vya maisha.

**Hitimisho**

Makala hii imejadili sababu za mhusika, Ngoma kuyajutia maisha yake katika riwaya ya *Ua la Faraja* (2004). Imebainika kwamba majuto yake yalitokana na aina ya maisha aliyochagua kuishi. Katika kuyasawiri maisha hayo, sababu kuu nne zimejadiliwa, yaani kukosa uaminifu katika ndoa, kuitelekeza familia yake, kuendekeza anasa, na kutowajali ndugu zake. Kwa jumla, mwandishi wa riwaya hii anamtumia Ngoma kusawiri maisha ya jamii ya Kitanzania na Kiafrika kwa jumla kutoa fundisho muhimu kwamba wazazi, hasa akina baba, wanapaswa kushiriki kikamilifu katika malezi ya watoto wao kwa kuwapa mahitaji muhimu. Kwa mujibu wa makala hii, wazazi au walezi wanaoshindwa kutimiza majukumu yao, huweza kuyajutia maisha yao wanapokumbwa na matatizo. Hii inatokana na ukweli kwamba matendo wafanyayo huweza kuathiri maisha yao ya baadaye.

**Marejeleo**

BAKITA, (2017). *Kamusi Kuu ya Kiswahili ya BAKITA*. Longhorn Publishers Ltd.
Madumulla, J. S. (1995). *Proverbs and Sayings: Theory and Practice*. TUKI.
Mieder, W. (2008). *Proverbs Speaks Louder than Words*. Peter Lang Publishing, Inc.
Mkufya, W. E. (2004). *Ua la Faraja*. Mangroove Publishers.
Mlacha, S. A. K. (1996). "Utamaduni wa Mwafrika katika Riwaya ya *Bwana Myombekere* na *Bibi Bugonoka". Mulika,* 23, pp. 24 – 35.
Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. KAUTTU.
Ponera, A. S. (2016). "Suala la Matumizi ya Nadharia kama Kiunzi cha Tafiti za Kitaamuli: Mfano wa Matumizi ya Nadharia ya Ukanivali". *Journal of Humanities*, Juz. 3, pp. 116 – 129.
TUKI. (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Oxford University Press.
Schlee, G. na Sahado, K. (2002). *Rendille Proverbs in their Social and Legal Context*. Rüdiger Köpper Verlag.
Wafula, R.M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. The Jomo Kenyatta Foundation.
Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Focus Books Publications Limited.
Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake*. Phoenix Publishers Limited.
Wanjohi, G. J. (2008). *The Wisdom and Philosophy of Gikuyu Proverbs*. Nyaturima Publications.